



# MWEZI WA DHUL-QA'ADA

**Mkusanyaji na Mkalimani:**

**Ummati Abdallah, Abuu Muhammad.**

**ILANI:**

**Saidia katika kukamilisha ujenzi wa Markaz Ibnu Uthaimin kwa kutoa sadaka yako kupitia mawasiliano yafuatayo:**

**MPESA : 0743 60 53 23**

**TIGO PESA : 0675 88 87 43**

**CRDB : 01334797708800**

Jina litakuja : Ibnu Uthaimin Islamiyah

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

**Sifa zote njema anastahiki Allah Mola Mlezi wa Ulimwengu. Na sala na salamu ziwe juu ya Mtume wetu Muhammad Swallallaahu alaihi wasallam, pamoja na watu wake na maswahaba wake wote.**

**Kwa kuwa tumo ndani ya mwezi wa Dhulqa'ada, pengine yafuatayo ni mojawapo ya maswali ya msingi kuyapatia majibu ndani ya mwezi huu tulionao;**

**(1) MWEZI WA DHUL-QA'ADA NI MWEZI GANI?**

**(2) KUNA UBORA NA FADHILA ZIPI NDANI YAKE?**

**(3) MAMBO GANI YA KUZINGATIA NDANI YAKE?**

**Risala hii fupi imekusanywa na kutarajamiwa kuhusu mwezi huu wa Dhul-qa'ada ili iwe ni ufupisho wenye kukusanya majibu ya maswali hayo.**

**Bila shaka, sababu kubwa ya kuandaa risala hii ni kupanua wigo wa ufahamu wangu katika kuifuatilia misimu ya mwaka mzimu kulingana na mwongozo wa Qur'an na Sunna kupitia ufahamu wa wema waliotangulia. Nataraji nitapata washiriki wenzangu katika kuhitajia kufahamu yaliyomo katika misimu hii ya mwaka, hivyo basi nimeifanya risala hii iwafikie pia ndugu zangu katika imani watakaokuwa na mahitajio kama mimi.**

**Risala hii fupi nimeigawa katika sehemu kuu tatu zifuatazo:**

**Sehemu ya kwanza:**

**Utambulisho wa Mwezi wa Dhul-qa'ada.**

**Sehemu ya pili:**

**Ubora na Fadhila za mwezi wa Dhul-qa'ada.**

**Sehemu ya tatu:**

**Mambo ya kuzingatia katika mwezi wa Dhul-qa'ada.**

**Tunamuomba Allah Mkarimu aturuzuku utakasifu wa nia zetu katika matendo yetu na ajaalie amali zetu ziwe sadaka zenye kuendelea malipo yake. Hakika yeye ndiye msimamizi wa hilo na muweza wa hilo.**

**Mkusanyaji na mkalimani:**

**Ummati Abdallah , Abuu Muhammad.**

## SEHEMU YA KWANZA:

## UTAMBULISHO WA MWEZI WA DHUL-QA'ADA.

**Mwezi wa Dhul-qa'ada ni mwezi wa kumi na moja katika kalenda ya Hijiria. Nao ni mwezi ambao upo katikati ya mwezi wa Shawwaal (mwezi wa kumi) na mwezi wa Dhulhijja ( mwezi wa kumi na mbili).**

**Umeitwa kwa jina hilo (Dhul-qa'ada) kwa sababu waarabu walikuwa wakiuheshimu na kuutukuza mno kiasi ambacho walikuwa wakikaa na kutulizana katika makazi yao pasina kutoka kwenda katika mapambano ya kivita na walikuwa pia wakiufanya ni mwezi wa maandalizi kwa ajili ya ibada ya Hajji.**

## SEHEMU YA PILI:

## UBORA NA FADHILA ZA MWEZI WA DHUL-QA'ADA.

### (1) DHUL- QA'ADA NI MWEZI KATIKA M I EZI M I TUKUFU.

**Mwezi wa Dhul-qa'ada ni miongoni mwa miezi mitukufu minne, mitatu yenye kufuatana ambayo ni Dhulqa'ada, Dhulhijja na Muharram; na mmoja uliojitenga peke yake ambao ni Rajab. Kama alivyosema Allah Mtukufu ; (( Hakika idadi ya miezi mbele ya ALLAH ni miezi kumi na mbili iliyopo kwenye makadirio ya Allah kuanzia siku alipoumba mbingu na ardhi; miongoni mwa hiyo kuna miezi minne mitukufu…)) Attauba 36**

**Kama ilivyo pia katika hadithi ya Mtume swallallaahu alaihi wasallam aliposema: (( ..Mwaka mmoja una miezi kumi na mbili; miongoni mwa hiyo kuna miezi minne mitukufu, mitatu yenye kufuatana ambayo ni Dhul-qa'ada na Dhul-hijja na Muharram, na Rajab mwezi wa Mudhari uliopo baina ya Jumaadah na Shaabaan.)) Bukhari na Muslim.**

**Miezi hii minne mitukufu, ukiwemo mwezi huu wa Dhul-qa'ada ni miezi yenye upekee mkubwa mbele ya ALLAH na ina nafasi kubwa mno kwa muislamu.**

### (2) DHUL- QA'ADA NI MWEZI KATIKA MIEZI YA HIJA.

**Amesema ALLAH Mtukufu : (( Ibada ya Hija ina miezi maalumu…)) Albaqarah 198; Amesema Ibnu Umar ALLAH amridhie ; (( Miezi (maalumu) ya Ibada ya Hija ni Shawwaal, na Dhul-qa'ada na Siku kumi za mwanzo za mwezi wa Dhul- hijja )) Taaliq ya Bukhari 2/141.**

### (3) INAPENDELEWA KUFANYA IBADA YA UMRA KATIKA MWEZI WA DHUL-QA'ADA.

**Hakika Mtume swallallaahu alaihi wasallam alifanya ibada ya umra mara nne na zote zilikuwa ndani ya mwezi wa Dhul-qa'ada; na wala hakufanya ibada ya umra ndani ya miezi mingine zaidi ya mwezi wa Dhul-qa'ada baada ya kuhama kwake kutoka Maka kwenda Madina. Umra ya kwanza ni Umra ya Hudaibiyah aliyoifanya mwaka wa sita katika mwezi wa Dhul-qa'ada, ya pili ni Umra ya Qadhaa aliifanya mwaka wa saba ndani ya mwezi wa Dhul-qa'ada, ya tatu ni Umra ya Ji'raana aliyoifanya mwaka wa nane ndani ya mwezi wa Dhul-qa'ada, ya nne ni Umra yake pamoja na ibada ya Haji mwaka wa kumi ndani ya mwezi wa Dhulqa'ada pia.**

**Kwa sababu hiyo wanazuoni wakasema kuwa, kufanya ibada ya umra ndani ya mwezi wa Dhul-qa'ada ni bora zaidi kuliko kuifanya katika miezi mingine yote isipokuwa mwezi wa Ramadhani. Japokuwa kuna baadhi ya wema waliotangulia kama vile Ibnu Umar na Aisha Allah awaridhie, wanaona kuwa kufanya ibada ya Umra ndani ya mwezi wa Dhul-qa'ada ni bora zaidi kuliko kuifanya katika miezi mingine hata Ramadhani.**

## SEHEMU YA TATU:

## MAMBO YA KUZINGATIA KATIKA MWEZI WA DHUL-QA'ADA.

### (a) KUZIDISHA KUFANYA MAMBO MEMA.

**Kwa kuzingatia kuwa mwezi wa Dhul-qa'ada ni miongoni mwa miezi mitukufu, tunatakiwa kuongeza kutenda wema katika yale ya faradhi juu yetu na hata yale ya sunna. Ndani ya miezi mitukufu (ukiwemo mwezi wa Dhulqa'ada) kuna ziada na ongezeko la malipo ya wema atakaoufanya muislamu, tofauti na wema atakaoufanya ndani ya miezi mingine isiyokuwa mitukufu. Hivyo basi, ni jukumu la kila muislamu kuitukuza miezi hii kwa kuongeza jitihada yake katika ibada zake.**

### (b) KUEPUKANA NA DHULMA ZA AINA ZOTE IKIWEMO USHIRIKINA NA MAASI MENGINE.

**Katika kuutukuza mwezi huu mtukufu wa Dhul-qa'ada tumekatazwa na sheria tusizidhulumu nafsi zetu ndani yake kwa kufanya ushirikina na madhambi mengineyo. Japokuwa dhulma haifai katika wakati na miezi mingine iliyobaki isiyokuwa mitukufu, lakini kuhusishwa katazo la dhulma ndani ya miezi hii mitukufu ni alama ya ongezeko la ubaya wa dhulma hiyo pindi itakapofanywa ndani ya mwezi wa Dhul-qa'ada na miezi mingine mitukufu. Hivyo basi, adhabu za dhulma hiyo huongezwa ukali wake endapo atatokea mtu katika sisi akawa jasiri wa kuvunja mipaka ya Allah ndani ya miezi aliyoitukuza mwenyewe ndani ya Qur'an na akakataza ndani yake dhulma. Kama alivyosema Allah Mtukufu ; (( Miongoni mwa hiyo miezi 12 , ipo miezi minne mitukufu, basi msizidhulumu nafsi zenu ndani yake )) Suurat Attauba 36.**

### (c) KUFANYA MAANDALIZI YA IBADA YA HAJI.

**Mwezi wa Dhul-qa'ada ni miongoni mwa miezi ya Ibada ya Haji. Hivyo wale wenye kiwango cha mali chenye kutosheleza safari yao ya kwenda Makka na kurudi pamoja na akiba ya matumizi ya familia zao, wajiandae kwa ajili ya safari hiyo. Na mojawapo ya maandalizi ya msingi yatakiwayo kwa watu hao ni kujitahidi kuisoma ibada ya Haji kwa kuhudhuria vikao vya kielimu vyenye kufundisha ibada hiyo sambamba na kuuliza maswali kwa wajuzi wa ibada hiyo.**

**MWISHO**

وصلى الله على محمد وعلى آله وصحبه وسلم

المراجع:


1) تفسير ابن كثير 4/147

2) تفسير الطبري 14/238

3) لسان العرب 3/ 357

4) صحيح البخاري

5) صحيح مسلم

6) مجموع فتاوى ابن باز 17/431

7) لطائف المعارف لابن رجب ص 259